**BUKU LA 15**

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb,

Jumatatu iliyopita, niliwasilisha taarifa ya Halmashauri ya Elimu ya Kaunti ya DeKalb (BOE). Majadiliano haya yalizingatia mahali tulipo katika mpango wetu wa kurudi katika masomo ya ana kwa ana.

Katika mkutano huo, nilishiriki na BOE kwamba maenezi ya COVID-19 katika jamii ya Kaunti ya DeKalb hayajapungua vya kutosha kusababisha wafanyakazi, waalimu, na wanafunzi kurudi katika masomo ya ana kwa ana. Kwa kuwa Wilaya imekuwa ikiwasiliana kwa mfululizo katika miezi michache iliyopita, kigezo chetu muhimu cha kwenda hatua ifuatayo katika mpango wetu wa kufungua tena ni kwamba ni lazima viwango vya maenezi katika jamii vipungue chini ya visa 100 kwa watu 100,000 kwa wastani wa siku 14. Tena, hatujawahi kuondoka kwenye mpango wetu ambao unahakikisha usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wetu ni wa maana.

Viashirio Vilivyotolewa na CDC vya Maelezo ya Kutoa Maamuzi ya Shule Mseto

| VIASHIRIAJI | Hatari ya Chini Zaidi ya Maambukizi katika Shule | Hatari ya Chini ya Maambukizi katika Shule | Hatari Wastani ya Maambukizi katika Shule | Hatari ya Juu ya Maambukizi katika Shule | Hatari ya Juu Zaidi ya Maambukizi katika Shule |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya visa vipya kwa watu 100,000 katika siku 14 zilizopita* | <5 | 5 hadi <20 | 20 hadi <50 | 50 hadi < 200 | >200 |
| Asilimia ya vipimo vya RT-PCR ambavyo vilipatikana kuambukizwa katika siku 14 zilizopita** | <3% | 3% hadi <5% | 5% hadi <8% | 8% hadi ≤ 10% | >10% |
| Uwezo wa shule kutekeleza mikakati 5 muhimu ya kupunguza hatari:<br>• Matumizi sahihi na ya mara kwa mara ya barakoa<br>• Kutokaribiana na watu ikiwa inawezekana<br>• usafi wa mikono na taratibu za kupumua<br>• Kusafisha na kuua vidudu<br>• Kuwafuatilia watu waliogusana kwa kushirikiana na idara ya afya ya nchini | Imetekeleza mikakati yote 5 kwa usahihi na kwa mfululizo | Imetekeleza mikakati yote 5 kwa usahihi lakini si kwa mfululizo | Imetekeleza mikakati 3-5 kwa usahihi na kwa mfululizo | Imetekeleza mikakati 1-3 kwa usahihi na kwa mfululizo | Haijatekeleza mikayoyote yoyote |

*Idadi ya visa vipya kwa watu 100,000 katika siku 14 zilizopita uhesabiwa kwa kuongezea idadi ya visa vipya katika kaunti (au aina nyingine ya jamii) katika siku 14 zilizopita vikigawanywa na idadi ya watu katika kaunti (au aina nyingine ya jamii) na kuzidisha kwa 100,000.

Nitaendelea kukutana na timu ya Ushauri wa Kimatibabu kuhusu COVID-19 ya DCSD ili kupitia mwongozo huu mpya uliosasishwa na kuanzisha maadili mema ya shughuli za shule salama wakati wa janga. Tunashirikiana pia na timu yetu ya matengenezo na vifaa ili kuhakikisha itifaki zinazofaa zimewekwa za mifumo ya usafiri na HVAC kabla ya shule kufunguliwa tena.

Jopo Kazi la COVID-19 la Kufungua Shule Tena hukagua tovuti ya GDPH kila siku baada ya saa 3:00 p.m ili kufuatilia data ya mtindo wa sasa ya Kaunti ya DeKalb na Georgia. Wilaya haihesabu data au kukisia kuhusu data inayoripotiwa na GDPH. Ikiwa ungependa kufikia maelezo haya, fuata hatua hizi:

1. Tembelea https://dph.georgia.gov/covid-19-daily-status-report baada ya 3:00 p.m. Kila siku ili utazame maelezo ya sasa.
2. Tembeze kwenye sehemu inayoonyesha ramani ya Georgia.

3. Elea juu ya Kaunti ya DeKalb ilu uone takwimu za kila siku.
4. Ikiwa ungependa kuona data ya historia, unaweza kubadilisha tarehe kwa kuchagua mwezi na siku kwenye menyu kunjuzi ya kalenda.

**Kushiriki kwa Jamii**
Asante kwa kila mtu aliyehudhuria Mkutano wa Mtandaoni wa Majira ya Kupukutika kwa Majani wa Baraza la PTA la DeKalb na hata pia katika Jumba Kuu la Jiji. Maoni na uwazi wenu ni wa maana na tutaendelea kuwa na mikutano zaidi ya mtandaoni ili kushiriki hatua kuhusu jinsi ya kuwaweka wafanyakazi na wanafunzi wetu salama. Isitoshe, shukrani maalum ziwaendee makamishna wetu Bi. Amanee Salahuddin na wanafunzi wake wa gredi ya kwanza katika Shule ya Msingi ya Flat Rock kwa kazi yao ngumu na kujitolea kwao kwa wanafunzi wetu.

**Ripoti Zilizokaguliwa za Fedha**
Ninafuraha kushiriki kwamba Wilaya ilipokea ripoti zilizokaguliwa za fedha kwa miaka ya kifedha ya 2018 na 2019. Ripoti hizo zinashiriki maoni wazi, yasiorekebishwa kuhusu shughuli za kifedha za Wilaya. Kuendelea kuboresha ukaguzi wetu wa kindani na michakato ya kuripoti ili kutoa uwazi wa fedha za Wilaya kumesalia kuwa kipaumbele muhimu kwangu na BOE.




**Fomu ya Nia ya Kurudi Shule** ilisambazwa mnamo Oktoba 9 Oktoba 9 ili wazazi/walezi waweze kuchagua chaguo lao wanalopendelea kwa kila mtoto. Majibu haya yataruhusu shule za nchini kuwapanga wanafunzi kwa makundi madogo ili kudumisha mahitaji ya kutokaribiana darasani wakati wa masomo mseto na kupanga wanafunzi ambao wataendelea kusoma mtandaoni nyumbani wakati Awamu ya III itaanza. Tafadhali bofya kwenye kiungo hapa chini ili ujaze Fomu ya Nia ya Kurudi Shule, ambayo inapatikana pia kwa lugha zetu kuu 15.

Kiungo: https://dekalb.co1.qualtrics.com/jfe/form/SV_cO7CQFP10BWfwuF

Ninajua familia nyingi zimeulizia kuhusu ni wapi wanaweza kupata taarifa kuhusu tunavyokabiliana na COVID-19 na kufunguliwa tena kwa shule. Hakikisha umepitia rasilimali hii, ambayo inaangazia njia tofauti ambazo tunatoa taarifa. Tunatoa pia chaguo za tafsiri za mawasiliano kwa wazazi ambao lugha yao msingi sio Kiingereza na uwezo wa kuchagua lugha inayopendelewa katika zana yetu ya Messenger ya Shule.

**Mabingwa Wapya wa Watoto**

Karibu wanatimu wetu wapya (Afisa Mkuu Mtendaji, Afisa Mkuu wa Fedha, na Msimamizi Msaidizi wa Kuwezesha Jamii, Uvumbuzi, na Ushirikiano ambao walijiunga nasi wiki iliyopita. Walitambulishwa kirasmi kwa timu zao mnamo Alhamisi, Oktoba 15, na tunafuraha kuwa nao ili kutuelekeza mbele.

**Wasomi Wetu**

Au'Niyah sasa ni sehemu ya Mpango wa Sanaa ya Mapishi ya Miller Grove. Alichaguliwa na mkufunzi wake na Wakfu wa Georgia wa Elimu ya Ukarimu (HEFG) ili kushiriki katika chajio ya kuchangisha fedha ya Kaunti ya DeKalb wiki iliyopita. Shukrani kwa Au'Niyah kwa kuwakilisha DCSD vizuri sana na kwa ufanisi wako unaoendelea katika mpango wa sanaa ya upishi. Inafaa hivyo!

Ningependa kutaja kwamba mnamo Oktoba 14, wanafunzi wetu wa gredi ya 10 na 11 walikuwa na nafasi ya kufanya PSAT/NMSQT. Shukrani maalum kwa wasomi, viongozi wa shule, na wasimamizi wote wa mitihani kwa mafanikio ya utekelezaji. Tungependa pia kushukuru idara yetu ya usafiri kwa kuwasafirisha wanafunzi wote waliosajiliwa na kuhakikisha wanafunzi walichukuliwa na kurudishwa kwa usalama katika kila shule. Utekelezaji wa pili wa PSAT/NMSQT utakuwa tarehe 29 Oktoba kwa wanafunzi waliosajiliwa. Tunatazamia utekelezaji salama na wa ufanisi wa 2 wa PSAT/NMSQT.

Ninashukuru kabisa kwa uvumilivu wenu tunapokuwa tukipitia mwaka huu wa masomo unaobadilika. Kama kawaida, ninaendelea kujitolea kwa usalama wa wanafunzi wetu na ufanisi wa elimu.

Shabiki wako wa #1,

Cheryl Watson-Harris